# MUUNGWANA OPEN SCHOOL
## TANGA
## P.O.BOX 778 TANGA
# FOMU YA KUJIUNGA NA SHULE

**WEBSITE: www.muungwanaopenschool.ac.tz**
**Email: info@muungwanaopenschool.ac.tz**
**INSTAGRAM, FACEBOOK, YOUTUBE, TWITTER: muungwana open school**
**SIMU NA: 0679565984 / 0685255998 /0714 -235246**

## YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE KIDATO CHA PILI(QT)

Tunakupongeza sana maana maamuzi yako ya kujiunga na Shule yetu ni miongoni mwa maamuzi bora kabisa uliyoyafanya 2023 kwani siyo tu yataamua maisha yako kielimu, pia yatachochea maendeleo yako binafsi na kutimiza ndoto zako.

Shule inatumia teknolojia ya kisasa katika *ufundishaji* na ujifunzaji wa wanafunzi, ina mazingira mazuri na tulivu ya kujifunza, madarasa ya kutosha, maktaba, maabara kwa masomo ya sayansi,mabweni ya wasichana na wavuilana, pamoja na vifaa vingine vingi vya kujifunzia, huduma ya kwanza pamoja na walimu wazoefu ambavyo vyote vina thibitisha kuwa maamuzi uliyo yafanya ya kujiunga katika shule hii ni maamuzi sahihi yatakayo timiza ndoto za maisha yako kwa ufanisi mkubwa kabisa

Muungwana Open School ndio shule bora kabisa hapa nchini Tanzania ambayo inatoa ELIMU HURIA katika program za:

**1. Elimu ya sekondari kidato cha I hadi IV (QT stage I&2) (Ordinary level) kwa wale walioikosa kutokana na changamoto mbalimbali.**
**2. kurudia mitihani ya Taifa kidato cha IV na VI (resiters)**
**3. Elimu ya kidato cha V na VI kwa mwaka mmoja ama miwili (QT stage three)**
**4. Elimu ya sekondari kidato cha I hadi VI kwa wale wenye sifa lakini hawakuchaguliwa katika shule za serikali**
**5. Pre-form five na Pre form one pamoja na twisheni za masomo ya sekondari kuanzia kidato cha I hadi VI**

Kila mwaka wanafunzi wetu wamekuwa wakifanya vizuri sana kwa kufaulu mitihani yao ya Taifa kwa kiwango cha juu kabisa na kusonga mbele katika level nyingine za elimu. Hii ni kwasababu shule ina sera mbalimbali ikiwemo ya usawa wa kijinsia pamoja na mbinu mahususi za wanafunzi kufanya vizuri.

Mwanafunzi akimaliza atapata cheti na sifa ambazo zitamsaidia kwenda katika kiwango kingine cha elimu.

### MAHALI SHULE ILIPO

Shule ipo Mkoa wa Tanga, Wilaya ya Tanga Mjini, kata ya Cental mtaa wa market sambamba na benki ya NMB Tawi la Madaraka umbali wa kilometa 8 Kutoka Stendi kuu ya Mabasi Kange, na mita 800 kutoka Stendi ndogo ya haisi (ngamiani) mjini, kutoka stendi kuu Kange na Stendi ndogo mjini nauli ya kufika shuleni ni shilingi mia nne (400) tu kwa mtu mzima na shilingi mia mbili (200) tu kwa Mwanafunzi.

## MASOMO YANAYOFUNDISHWA HAPA SHULENI

Shule inaendesha program katika michepuo yote (Sayansi, Sanaa na Biashara) katika masomo na tahasusi (combination) zote kama

Basic Mathematic, Physics, Chemistry, Biology, Geography, History, English Language, Literature in English, Kiswahili, Civic, Commerce, Book Keeping na Account

# SARE YA SHULE

- Sare ya shule kwa wanafunzi wa  kidato cha kwanza hadi cha nne, **wasichana** na **wavulana** ni sketi au suruali rangi ya DAMU YA MZEE (DACK) na shati jeupe la mikono mifupi AMA short kanzu yenye ufito wa rangi ya sketi kwenye mikono na  mtandio mweupe ama hijabu nyeupe.na tai ya rangi ya suruali ama sketi na viatu vyeusi vya kufunika.
- Wanafunzi wa kidato cha V na VI ni suruali ama sketi ya kijani na shati nyeupe ya mikono mirefu na tai ya rangi ya suruali ama sketi.
- Tshirt ya shule inapatikana shuleni kwa shilingi 15,000/=.

## SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

### A. SHERIA

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu (TEWW) ya Bunge No.12 ya mwaka 1975 iliyoanzishwa na Bunge tuna zingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini, unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yamefafanuliwa hapa chini.

a) Kulipa ada na michango yote mapema na kwa mihula kama ilivyo elekezwa kwenye fomu hii

b) Mwanafunzi anapaswa kuvaa sare ya shule wakati wote awapo shuleni na akienda nyumbani.(wa asubuhi)

c) Mwanafunzi anapaswa kuwa mahudhurio mazuri katika shughuli za nd   ani na nje ya darasa kama itavyo elekezwa na shule.

d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hii

e) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.

g) Wanafunzi wanatakiwa kuwa mfano mzuri kwa heshima na tabia kwa kauli na vitendo vyao.

h) Ni marufuku kwa mwanafunzi kutumia lugha chafu au ya kihuni popote na wakati wowote awapo shuleni.

i) Ni marufuku kuvuta sigara au kutumia madawa ya kulevya uwapo shuleni.

j) Marufuku kwa mwanafunzi kutukana kumpiga au kupigana na mwanafunzi mwenzake au mwalimu

k) Mwanafunzi asipige kelele anapokuwa darasani.

l) Mwanafunzi anapaswa kuzingatia ratiba yashule wakati wote

m) Mwanafunzi wa asubuhi haruhusiwi kuja wala kutumia simu,I-pad, mp3 hapa  shuleni ama hostel mwanafunzi akionekana na vitu hivyo atafukuzwa shule haraka.

n) Ni lazima kwa mwanafunzi kutumia lugha ya kiingereza wakati akiwa kwenye mazingira ya shule.

o) Wanafunzi hawaruhusiwi kuvaa vitu vya samani kama gold,silva nk

p) Mwanafunzi wa kutwa ataruhusiwa kuondoka shuleni kurudi nyumbani pale tu ratiba ya shule inapoisha ama kama amepata dharura.

q) Wanafunzi wa hostel wataruhusiwa kutembelewa na wazazi siku ya jumapili ya wiki tu.

r) Mwanafunzi atalazimika kufanya mitihani ya wiki, mwezi,mock, pre national na mazoezi mengine kama ratiba za shule zitavyo eleza.

s) Mwanafunzi ambaye hayupo shule bila taarifa yeyote shuleni kwa kipindi cha mwezi mmoja atakuwa amejifukuzisha shule mwenyewe na hatopokelewa tena shuleni.

t) Mawasiliano ya wanafunzi kwa wazazi au walezi wao yatafanyika kupitia simu ya Matron au Patron ama simu ya shule.

u) Mwanafunzi wa bweni haruhusiwi kuleta ndugu,rafiki ama mtu yeyote kwenye mazingira ya shule bila ya taarifa kutoka uongozi wa shule.

v) Mwanafunzi wa bweni haruhusiwi kutoka nje ya shule bila ya ruhusa kutoka kwa mwalimu ama uongozi wa shule.

**B) MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWASHULE**

1. Mahudhurio hafifu darasani ambayo yatapunguza tija kwa mwanafunzi kufanya vizuri katika mitihani yake.
2. Wizi ,uasherati, ubakaji au ushoga.
3. Kupigana au kumpiga mwanafunzi ama mwalimu.
4. Kuvuruga amani shuleni
5. Kutolipa ada ya shule kwa wakati.
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya mtu au ya shule
5. Kuvunja sheria za shule
6. Mwanafunzi wa masomo ya asubuhi kuja na **SIMU YA MKONONI, I-PAD AU MP3 SHULENI**
7. Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya.
8. Makosa ya jinai.
9. kuchochea na kuvuruga amani ya shule.
10. Kitendo chochote kinacho idharirisha na kushusha ama kuharibu taswira ya shule.
11. Kuja na silaha ama kuitumia kudhuru watu wengine.
12. Kutoka nje ya shule bila ya ruhusa.

# ADA (KARO) YA SHULE

Ada ya masomo kwa mwaka mzima ili kuleta urahisi kwa mzazi ama mlezi katika malipo imegawanywa katika awamu nne kwa kidato cha pili (QT), kama ifuatavyo:

## MWANAFUNZI WA KUTWA KIDATO CHA PILI (QT) TSHs. 650,000/=

| AWAMU YA 1 | AWAMU YA 2 | AWAMU YA 3 | AWAMU YA 4 |
|---|---|---|---|
| Jan-March | April -May | June -July | August-Sept |
| 250,000/= | 200,000/= | 150,000/= | 50,000/= |

## MWANAFUNZI WA BWENI KIDATO CHA PILI (QT) 1,750,000

| AWAMU YA 1 | AWAMU YA 2 | AWAMU YA 3 | AWAMU YA 4 |
|---|---|---|---|
| Jan-March | April -May | June -July | August-Sept |
| 500,000/= | 500,000/= | 450,000/= | 300,000/= |

**OFA:** WATAKAOLIPA KUANZIA SHILINGI **350,000/=** NA RIMU 2 WATAPATA OFA ZIFUATAZO: - ENGLISH COURSE MIEZI 6, SARE ZA SHULE, MADAFTARI 3 (counter books) NA KALAMU **BURE** PIA KIASI KINACHOBAKIA MZAZI ANAWEZA KULIPA SHILINGI 100,000/= (LAKI MOJA) KWA KILA MWEZI KWA WANAFUNZI WA KUTWA.

**KWA**

WANAFUNZI WA BWENI WATAKAOLIPA KUANZIA SHILINGI **600,000** PAMOJA NA RIMU 2 PIA WATAPATA OFA ZILIZOTAJWA HAPO JUU. PAMOJA NA KULIPA SHILINGI **190,000** /= KWA KILA MWEZI.

- **TSHIRT INAPATIKANA SHULENI KWA SHILINGI 15,000/= TU.**
-

**MALIPO YOTE YAFANYIKE BENKI AU KWA WAKALA KUPITIA AKAUNTI NAMBA 41710053799 NMB: MUUNGWANAOPEN SCHOOL.**

**AU LIPA KWA TIGO PESA 7053604 MUUNGWANA OPEN SCHOOL.**

**ZINGATIA: HATUPOKEI PESA TASLIM SHULENI.**

Ukifanya malipo kupitia benki au kwa wakala kwenye akaunti namba tajwa hapo juu. Unapaswa kurejesha nakala (payslip) ya malipo yako hapa shuleni nakupatiwa risiti ya shule.

## SIFA NA MAHITAJI YA USAJILI WA WANAFUNZI KIDATO CHA PILI (QT)

1. Mwanafunzi atasajiliwa kusoma kidato cha QT kama alifanya mtihani wake wa Taifa wa darasa la saba
2. Mwanafunzi awe anajua kusoma na kuandika kwa ufasaha.
3. Awe alifanya mtihani wa maarifa (QT) lakini hakufaulu vizuri
4. Awe alimaliza kidato cha nne ama hakufanikiwa kumaliza kwa sabababu ya changamoto mbalimbali.
5. Mwanafunzi anapaswa kuwa na kamusi/Dictionary kwajili ya kujifunza lugha ya kiingereza.
6. Mwanafunzi anapaswa kuleta matokeo yake aliyoyapata kwenye mtihani wa awali ama kuleta namba sahihi aliyotumia wakati akifanya mtihani huo.

## MAHITAJI YA WANAFUNZI WA BWENI

1.Mwanafunzi anapaswa kuja na godoro dogo futi $2^{1}/_{2}$
2.Chandalua(net) ya futi tatu kwa sita
3. Ndoo ndogo moja kwajili ya kufulia na kuogea
4.Viatu vya kuogea (malapa/yeboyebo)
5. Shuka mbili za rangi yeyote
6.Vyombo vya chakula kama sahani au kontena,kikombe cha chai,kijiko nk
7.Nguo za michezo kama traksuti na viatu
8.Vitu vingine kama mswaki,dawa meno,sabuni,mto wa kulalia, nk

## SHERIA ZA BWENI

1.Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki wala kutumia simu wa radio bwenini
2.Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya bweni kwenda mitaani bila ya ruhusa ya shule.
3.Mwanafunzi haruhusiwi kuchkua/kuiba kitu chochote cha shule au cha mwanafunzi mwenzie.
4.Mwanafunzi haruhusiwi kupiga kelele usiku wakati wa kulala.
5.Mwanafunzi anapaswa kuzingatia ratiba ya kufanya usafi kama ilivyo pangwa na kiongozi wa bweni
6.Mwanafunzi anapaswa kumuheshimu patron/matron na kutii maagizo yote halali yanayotolewa na viongozi wa mabweni pamoja na walimu.
7.Mwanafunzi anapaswa kuingia vipindi vyote vya kujisomea usiku kuanzi saa 2 kamili hadi saa 4 na nusu usiku kama ilivyo pangwa na shule.

## VIAMBATISHO “A” , “B” NA “C” VINATAKIWA VIJAZWE NA VIRUDISHWE SHULENI

**KIAMBATISHO**

**A: KIJAZWE NA MWANAFUNZI:**
**B: KIJAZWE NA MZAZI / MLEZI**
**C: FOMU YA KUJIUNGA NA SHULE**

**“A”**

**AHADI YA MWANAFUNZI:**

MUUNGWANA OPEN SCHOOL,
P.O.BOX 778,
TANGA.
Email:info@muungwanaopenschool.ac.tz

**YAH: KUKUBALI KUFUATA SHERIA NA MASHARTI YA SHULE**

Mimi………………………………………………………………nakubali nafasi ya Kidato cha …………… niliyopewa katika shule yako ya Muungwana Open Scool. Nayakubali masharti yote kuwa nitatii sheria za shule kama zilivyo orodheshwa hapo juu na zile zitakazotolewa kwa muda wote wa masomo yangu.

Naahidi kuwa nitawaheshimu na kuwatii Walimu wote wa shule na wafanyakazi wote kama walezi wangu.**NAAHIDI KULIPA KARO YA SHULE KAMA ILIVYO ELEKEZWA**

Naahidi kuwa nitatii wale wote watakao teuliwa kuchaguliwa kuwa Viongozi wangu kwa mujibu wa sheria za shule.

Naahidi kuwa nitakuwa mwanafunzi mwaminifu na naahidi pia kuwa nitajielimisha kwa nguvu zangu na akili zangu zote kwa manufaa yangu binafsi na Taifa langu.

**JINA LA MWANAFUNZI:…………………………………………………............**

**SAHIHI:……………………………….**

**NAMBA YA SIMU YA MWANAFUNZI: ………………………………….....……**

**KWA MATUMIZI YA OFISI TU:**
**JINA LA AFISA: ________________________________SAHIHI: _______TAREHE: ______**

**"B"**

## AHADI YA MZAZI/MLEZI

MUUNGWANA OPEN SCHOOL,
P.O.BOX 778,
TANGA.
Email: info@muungwanaopenschool.ac.tz

1. Jina la Mzazi/Mlezi ___________________________
2. Kazi _______________________________________
3. Simu ____________________
4. Mahali ninapoishi________________________

**AHADI YA MZAZI / MLEZI YA KULIPA KARO NA MICHANGO YA SHULE:**
Mimi_______________________________Mzazi /Mlezi wa ________________________ wa **Kidato cha______ mwaka 2022** katika **Shule ya Muungwana Open School**. Nathibitisha na kuahidi kuwa nipo tayari kulipa **KARO** ya shule pamoja na michango mingine kama ilivyo idhinishwa na shule kwa ajili ya maendeleo ya shule na wanafunzi.
Pia naahidi kuwa kila ifikapo mwisho wa **Muhula wa Shule** (**Mwezi _____**au______) Nitakuwa nimemamiliza kulipa kiwango kilicho wekwa.

**TAARIFA KUHUSU AFYA YA MWANAFUNZI**

JE MWANAFUNZI ANA MATATIZO YOYOTE KIAFYA?

Andika neno **NDIO** au **HAPANA** kama mtoto ana matatizo haya au la

(a)Uoni hafifu____________

(b)Matatizo ya kusikia___________

(c)Matatizo ya kuongea_________

(d)T.B__________

(e)Presha________

(f)Ana ulemavu wowote unao athili taaluma________

g) sikle cells

(h) Au kama anatatizo lolote lingine_______

**SAINI YA MZAZI/ MLEZI_____________TAREHE________________**

**KWA MATUMIZI YA OFISI TU:**

**JINA LA AFISA_____________________________________CHEO:_____________________**

**SAHIHI___________________TAREHE:** ____________

**"C"**

# MUUNGWANA OPEN SCHOOL

PASSPORT

## FOMU YA KUJIUNGA NA SHULE

**P.O.BOX 778 - TANGA**

**SIMU NA: 0679565984 / 0685255998 /0714 -235246**

**Email: info@muungwanaopenschool.ac.tz**

### TAARIFA ZA MWANAFUNZI

| | | | |
|---|---|---|---|
| JINA KAMILI | | | |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| TAREHE YA KUZALIWA | | | | | | | | |

| | |
|---|---|
| JINSIA | |

| | |
|---|---|
| NAMBA YA SIMU | |

| | |
|---|---|
| DINI | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| MAHALI UNAPOTOKA | MKOA | WILAYA | MTAA/KIJIJI |
| | | | |

### TAARIFA YA MZAZI

| | | | |
|---|---|---|---|
| JINA LA BABA/MAMA | | | |

| | |
|---|---|
| NAMBA YA SIMU | |

| | |
|---|---|
| KAZI | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| MAHALI UNAPOTOKA | MKOA | WILAYA | MTAA/KIJIJI |
| | | | |

### TAARIFA YA MLEZI

| | | | |
|---|---|---|---|
| JINA KAMILI | | | |

| | |
|---|---|
| NAMBA YA SIMU | |

| | |
|---|---|
| KAZI | |

| | |
|---|---|
| UHUSIANO | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| MAHALI UNAPOTOKA | MKOA | WILAYA | MTAA/KIJIJI |
| | | | |